

Ndalichako: Acheni siasa katika kusimamia maadili shuleni.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako ameziagiza mamlaka zinazohusika na elimu nchini kuacha siasa na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinaposimamia maadili ya wanafunzi shuleni

Waziri Ndalichako alitoa agizo hilo hivi karibuni jijini Dar es Salaam wakati akifungua mdahalo kuhusu kujenga na kukuza maadili, haki za binadamu, uwajibikaji, utawala Bora na mapambano dhidi ya rushwa.

Waziri Ndalichako amesema, “usimamizi wa maadili shuleni usitawaliwe na siasa, bali wahusika wahakikishe wanazingatia sheria, kanuni, taratibu na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na serikali.”

Aidha Waziri huyo ameongeza kuwa, “wanafunzi zingatieni matendo mema, kuweni wasikivu, zingatieni mafundisho na epukeni maovu kwa sababu msipofundishika serikali hata ikiwalipia ada, itakuwa ni kazi bure.”

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, suala la mmomonyoko wa maadili hivi sasa ni kubwa sana, hivyo amewaagiza wanafunzi walioudhuria mdahalo huo kuwa mabalozi wazuri wa maadili kwa vijana mitaani.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam Sheikh Ali Mbwela aliwataka wanafunzi kuwa na maadili ili kuliepushia taifa matatizo.

Shehe Mbwela amesema, “wanafunzi zingatieni maadili ya nchi yetu. Msipokuwa na maadili mtakuwa mzigo mkubwa kwa walimu, wazazi na jamii kwa ujumla.”

Kiongozi huyo wa dini aliongeza kuwa ukosefu wa maadili kwa vijana utawasababishia matatizo makubwa, watataabika, watateseka na kuliletea Taifa matatizo ya kila aina.

Baadhi ya madhara yanayosababishwa na ukosefu wa maadili yaliyotajwa na washiriki wa mdahalo huo ni vijana wasio na maadili kutohaminiwa katika jamii, kukosa ajira utokana na kuwa na tabia mbaya,, kukosa fursa za kujiendeleza kielimu na kulisababishia taifa migogoro ya mara kwa mara.

Mdahalo huo umeandaliwa na taasisi zinazohusika na masuala ya utawala bora ikiwemo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB), Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA) na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

Taasisi nyingine ni Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Umma na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mdahalo huo uliwashirikisha wanafunzi kutoka shule 20 za msingi na sekondari mkoani Dar es Salaam.

Mdahalo huo ni mwendelezo wa kampeini ya kitaifa ya Maadhimisho ya siku ya Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora, na Mapambano dhidi ya Rushwa nchini.

Kauli mbiu ya maadhimisho hayo mwaka huu ni ***Kujenga na Kukuza maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa.***